ISSN (Online): 2455-3662
EPRA International Journal of Multidisciplinary Research (IJMR) - Peer Reviewed Journal
Volume: 11| Issue: 8| August 2025|| Journal DOI: 10.36713/epra2013 || SJIF Impact Factor 2025: 8.691 || ISI Value: 1.188

# CHANGAMOTO NA FAIDA ZA KUFUNDISHA KISWAHILI MKONDONI KATIKA VYUO VIKUU VYA KENYA UTANGULIZI

**Rhoda Kawira[1], Dr. Sarah Ndanu M. Ngesu[2], Dr. Esther Chomba[3]**
[1]*Mwanafunzi wa Uzamili, Kitivo Cha Elimu, Chuo Kikuu Cha South Eastern Kenya*
[2]*Kitivo Cha Elimu, Chuo Kikuu Cha South Eastern Kenya*
[3]*Kitivo cha Elimu,Chuo Kikuu cha South Eastern Kenya*

## IKISIRI

*Utafiti huu ulilenga kutathmini Changamoto na Faida za Kufundisha Kiswahili Mkondoni katika Vyuo Vikuu vya Kenya. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya mawasiliano iliyoasisiwa na wanaisimu Firth, Halliday na Hymes mnamo mwaka wa 1980. Wanaisimu wengine kama vile Naom Chomsky walichangia na kuendeleza nadharia hii. Mbinu za ukusanyaji data zilizotumika ni mahojiano na ujazaji wa hojaji. Waliotoa taarifa waliteuliwa kimakusudi ili waweze kusaidia katika kupata data iliyohitajika. Wanafunzi wanaosoma somo la Kiswahili wa mwaka wa kwanza, pili, tatu na nne wanaofanya kozi ambazo walimu hutumia teknolojia kufundisha walihusishwa. Hii ni kwa sababu si kozi zote zinazofundishwa mkondoni. Wanafunzi wa uzamifu na uzamili, ambao wanafanya kozi ya Kiswahili, pia walihusishwa. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kitaamuli na kitakwimu na kuwasilishwa kwa michemihimili na micheduara. Walimu watano wanaojihusisha na ufundishaji wa Kiswahili mkondoni pia walihusishwa katika kutoa habari.Hii ni kwa sababu wako na tajiriba katika ufundishaji huo.*

**MANENO MUHIMU:** *Masomo, Mkondoni, Teknolojia, UVIKO 19.*

## UTANGULIZI

Janga la UVIKO -19 liliathiri kwa kiasi kikubwa jamii, uchumi na sekta ya elimu kote duniani. Kufuatia kufungwa kwa taasisi za elimu, Wizara ya Elimu na Michezo (WEM) ilianzisha programu za kujifunza kwa njia ya mtandao. Hatua hii ilisaidia kuendeleza shughuli za ufundishaji na ujifunzaji, zikiwemo za somo la Kiswahili. Kupitia teknolojia ya mtandao, walimu waliweza kuwafikia wanafunzi wengi kwa wakati mmoja na kuendesha vipindi vya masomo kwa urahisi zaidi.

Ingawa teknolojia imeshatumika katika ufundishaji wa Kiswahili, hususan katika vyuo vikuu, bado kuna uhaba wa maarifa kuhusu mbinu hii ya ufundishaji. Sera ya Kitaifa ya Elimu (NPE) inasisitiza kuwa "uelewa wa kidijitali" ni sehemu muhimu ya ukuzaji wa mwanafunzi, uraia, na ajira katika jamii za kisasa. Hata hivyo, ufundishaji wa Kiswahili mtandaoni unakumbwa na changamoto mbalimbali.

Utafiti wa awali ulibainisha kuwa baadhi ya wahadhiri waliepuka kutumia mbinu hii, hasa katika kiwango cha shahada ya kwanza, wakiiangazia zaidi kwa wanafunzi wa shahada ya uzamili. Kwa mujibu wa Ogott na Odera (2012), miundombinu duni na ukosefu wa mafunzo kwa walimu ni miongoni mwa sababu zinazowafanya wahadhiri kusitasita kutumia teknolojia katika ufundishaji. Ufundishaji wa mtandaoni unazingatiwa kuwa nyenzo muhimu ya maendeleo ya elimu kwa kuwa unamwezesha mwanafunzi kupata mafunzo popote na wakati wowote bila kufungika kwa mazingira ya darasani.

Ingawa tafiti nyingi zilibainisha umuhimu wa ufundishaji mtandaoni wakati wa janga la UVIKO -19, kuna utafiti mchache unaolenga moja kwa moja ufundishaji wa Kiswahili kwa njia ya mtandao. Haijabainika kwa kina jinsi somo la Kiswahili hufundishwa mtandaoni, changamoto zinazojitokeza na mikakati ya kukabiliana nazo. Kwa hivyo, utafiti huu ulilenga kutathmini matumizi ya teknolojia katika ufundishaji wa Kiswahili.

Ngesu (2020) alisisitiza umuhimu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni, akitaja zana kama tafsiri za kimitambo, kompyuta na kamusi za kielektroniki. Mohochi (2016) alieleza kuwa lugha za Kiafrika, zikiwemo Kiswahili, zinawakilishwa kidogo katika ufundishaji wa lugha kwa njia ya kidijitali ikilinganishwa na lugha za kigeni kama Kifaransa, Kijapani na Kijerumani. Watafiti wengine kama Johan (1992) na Kramch (2014) walihimiza umuhimu wa kuunganisha TEHAMA katika ufundishaji wa lugha ili kukabiliana na changamoto za kitamaduni kama vile uhaba wa walimu na vifaa vya kujifunzia.

### Ujifunzaji Mtandaoni

Kwa mujibu wa Adnan na Anwar (2020), ujifunzaji wa mtandaoni hauwezi kufanikishwa ipasavyo katika baadhi ya nchi kama Pakistan kwa sababu walimu na wanafunzi hawana ujuzi wala rasilimali za kushiriki masomo mtandaoni.

Katika utafiti uliofanyika nchini India, matatizo kadhaa yaliibuka. Nambiar (2020) alifanya utafiti kuhusu kuhamasisha walimu na wanafunzi kukubali ujifunzaji wa mtandaoni wakati wa janga la UVIKO -19. Washiriki wa utafiti walikuwa wanafunzi 407 na wahadhiri 70 kutoka vyuo vya Bangalore. Matokeo yalionyesha haja ya kuwepo kwa mwingiliano thabiti kati ya wanafunzi na walimu. Utafiti huo pia ulisisitiza umuhimu wa kuwa na mfumo

ISSN (Online): 2455-3662
EPRA International Journal of Multidisciplinary Research (IJMR) - Peer Reviewed Journal
Volume: 11| Issue: 8| August 2025|| Journal DOI: 10.36713/epra2013 || SJIF Impact Factor 2025: 8.691 || ISI Value: 1.188

uliopangiliwa vizuri ili kutoa mazingira mwafaka kwa elimu ya mtandaoni. Hatimaye, utafiti huo ulihitimisha kwa kusisitiza umuhimu wa kutoa mafunzo kwa walimu ili wawe na ujuzi wa kutosha wa kufundisha kwa njia ya mtandao.

Utafiti huu una umuhimu kwa utafiti wa sasa kwa kuwa unachunguza masuala ya ujifunzaji wa mtandaoni na unahusisha walimu na wanafunzi, kama ilivyo kwa utafiti unaopendekezwa. Hata hivyo, tafiti zinatofautiana kwa kuwa utafiti wa Nambiar (2020) ulilenga kuwahamasisha walimu na wanafunzi kuukubali ujifunzaji wa mtandaoni, huku utafiti wa sasa ukilenga kutathmini ufundishaji wa Kiswahili kama mojawapo ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji.

Utafiti wa awali ulifanyika katika mazingira ya India, tofauti na utafiti wa sasa utakaofanyika Kitui, Kenya.

Vivyo hivyo, Babar (2020) alichunguza mitazamo ya wanafunzi kuhusu ujifunzaji wa mtandaoni wakati wa janga la UVIKO -19 nchini India na Korea Kusini. Aligundua kuwa wanafunzi walipendezwa na ujifunzaji wa mtandaoni kwa sababu uliwapa nafasi ya kushirikiana, uliwavutia kupenda masomo, uliwawezesha kuelewa vizuri kazi zao za darasani, na walifurahishwa na namna walimu walivyotoa mafunzo. Kwao, mbinu hii ilikuwa ya manufaa na ilikidhi mahitaji ya elimu ya mtandaoni.

Utafiti huu unachangia utafiti wa sasa kwa kuwa unaangazia mitazamo ya wanafunzi, sawa na utafiti unaopendekezwa. Hata hivyo, utafiti wa Babar (2020) ulilenga mitazamo ya wanafunzi pekee kuhusu ujifunzaji wa mtandaoni, ilhali utafiti wa sasa unahusisha walimu na wanafunzi ili kupata taarifa kuhusu ufundishaji wa Kiswahili kwa njia ya mtandao.

Katika utafiti uliofanyika Palestina, Farrah na Al Bakry (2020) walichunguza mitazamo ya wanafunzi waliokuwa wakijifunza Kiingereza kama lugha ya kigeni (EFL) katika vyuo sita vya Palestina kuhusu ujifunzaji wa mtandaoni wakati wa janga la UVIKO -19. Watafiti hao walibaini kuwa wanafunzi walitambua faida nyingi za ujifunzaji wa mtandaoni. Pia walibaini changamoto mbalimbali walizokumbana nazo wakati wa mabadiliko kutoka kwa mbinu za jadi hadi mtandaoni. Zaidi ya hayo, walitoa mapendekezo kuhusu namna ya kuboresha mbinu za ufundishaji mtandaoni kama vile kutoa rasilimali muhimu na kuwapa walimu na wanafunzi ujuzi unaohitajika ili kuwezesha ujifunzaji unaofaa.

Utafiti wao unachangia utafiti wa sasa kwa kuwa unahusiana na ujifunzaji wa mtandaoni, sawa na utafiti huu. Hata hivyo, ulikuwa wa jumla na haukulenga somo maalum. Kila somo lina upekee wake, na ni muhimu kuchunguza mbinu mahususi zinazotumika kulifundisha. Hali hii imechochea utafiti wa sasa kuangazia kwa kina ufundishaji wa Kiswahili kwa njia ya mtandao.

Aidha, Farrah na Al Bakry walifanya utafiti wao katika vyuo vya Palestina, tofauti na utafiti wa sasa unaofanyika katika chuo kikuu cha Kenya katika muktadha wa Kiafrika unaotofautiana na ule wa Palestina. Pia, utafiti wao ulihusisha kipindi mahsusi cha janga la UVIKO -19, huku utafiti wa sasa ukichunguza hali ya sasa ambapo ujifunzaji wa mtandaoni umeendelea hata baada ya janga hilo. Vilevile, hawakulenga masomo mahsusi bali walichunguza ujifunzaji kwa ujumla. Kwa hivyo, utafiti huu wa sasa unatarajiwa kuleta matokeo tofauti na kutoa maarifa mapya kuhusu ufundishaji wa Kiswahili mtandaoni

**Tafiti kuhusu Nafasi ya Teknolojia Katika Ufundishaji wa Kiswahili**

Ngesu (2020) katika utafiti wake, alitathmini kuhusu nafasi ya teknolojia ya habari (TEHAMA) na mawasiliano katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Katika utafiti wake anaeleza kuwa, matumizi ya TEHAMA yanahusu uwezo wa kutumia chombo au kifaa chochote cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kufundishia lugha za kigeni (LG) kama vile Kiswahili. Malengo ya utafiti huo yalikuwa kutathmini nafasi ya vifaa mbalimbali vya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kwamba matumizi ya tafsiri mashine, tarakilishi, mtandao na kamusi za kieletroniki yana mchango mkubwa katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni.

Hata hivyo, utafiti wa Ngesu (2020) unatofautiana na wa sasa kwa kuwa ameangazia lugha ya Kiswahili kama lugha ya kigeni, kwa wajifunzaji ambao hawapati ingizo kutoka kwa jamii kwa kuwa haizungumzwi katika maisha ya wanajamii ya kila siku. Aidha, wajifunzaji waliolengwa katika utafiti wake walikuwa wa jumla mradi wawe wanajifundisha lugha ya Kiswahili kama lugha ya kigeni. Utafiti unaopendekezwa, unaangazia ufundishaji wa Kiswahili mkondoni kwa kuwaangazia wanafunzi wa chuo kikuu nchini Kenya wanaojifundisha Kiswahili kama lugha ya pili ambayo inazungumzwa na wanajamii nje ya darasa. Pia, utafiti wa awali umeegemea kigezo cha TEHAMA, ilhali utafiti wa sasa utajikita katika ufundishaji wa mkondoni. Hivyo, inatarajiwa kwamba utafiti unaopendekezwa utakuwa na matokeo tofauti na kuchangia maarifa mapya.

Kwa mujibu wa wataalamu Johan (1992), Maw (1999), Safari (2012) Kramch (2014), Mohochi (2016) na Michira (2017), kwa miaka 10 iliyopita, ulimwengu umeshuhudia matumizi makubwa ya teknolojia ambayo yana athari hasi katika ufundishaji wa lugha za kigeni. Aidha, maendeleo katika jamii kwenye karne hii ya 21 yanahimiza kuwapo kwa ubunifu katika mchakato wa ufundishaji unaotilia maanani utangamano wa wanafunzi wote duniani. Ufundishaji wa Iugha katika sehemu nyingi duniani hukabiliwa na changamoto kama vile ukosefu wa walimu waliofuzu, ukosefu wa vitendea kazi pamoja na kutokubalika kwa mbinu nyinginezo za ufundishaji (Mathew, 1992). Kulingana na Bilyalova (2017), njia mojawapo ya kukabiliana na changamoto za ukosefu wa walimu wa kutosha, ukosefu wa vitendeakazi vya ufundishaji na matumizi ya mbinu changamani katika ufundihaji wa lugha za kigeni ni matumizi ya TEHAMA. Altun (2015) kuhusu suala hili anaeleza kwamba TEHAMA ni zana muhimu katika ufundishaji kwa kuwa huwapa motisha wanafunzi na kulifanya somo kuvutia na kufurahiwa na wanafunzi wote. Kwa mujibu wa Shin (2015), maendeleo ya teknolojia yamepanua matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa lugha, Katika kame hii ya 21 walimu wa lugha wanatakiwa kuwa na uelewa wa kutumia TEHAMA kama

ISSN (Online): 2455-3662
EPRA International Journal of Multidisciplinary Research (IJMR) - Peer Reviewed Journal
Volume: 11| Issue: 8| August 2025|| Journal DOI: 10.36713/epra2013 || SJIF Impact Factor 2025: 8.691 || ISI Value: 1.188

vile kompyuta na mtandao kama mbinu ya ufundushaji ili kufanikisha ufundushaji wa LG. Nchi mbalimbali kama vile Korea zimeanzisha programu za kuwafundisha walimu wa lugha jinsi ya kutumia kompyuta ambayo ni kipengele kimojawapo cha TEHAMA katika ufundushaji wa lugha ya Kiingereza.

Mohochi (2016) katika utafiti aliofanya kuhusu ufundishaji wa Kiswahili kupitia teknolojia anaeleza kwamba mbinu hii haijapewa nafasi inayostahiki. Aidha, Mohochi anasema kuwa lugha za nje kama vile Kijapani, Kifaransa, Kichina na Kijerumani hufundishwa kwa upana kidijitali kuliko lugha za Kiafrika kikiwamo Kiswahili. Isitoshe, programu nyingi za vyuo vya walimu zimetambua umuhimu wa kutumia TEHAMA katika ufundishaji wa LG. Vifaa vya TEHAMA vinavyoweza kutumiwa katika ufundishaji wa Kiswahili ni kama vile: kompyuta, mtandao (mkondoni), televisheni, simu za kiganjani, redio na kadhalika.

Hata hivyo, utafiti wa Mohochi (2016) umeshughulikia ufundishaji unaokitwa kwenye kompyuta. Lengo la utafiti wake lilikuwa kufafanua nafasi ya TEHAMA kama nyenzo muhimu katika ufundishaji wa Kiswahili tofauti na utafiti unaopendekezwa ambao unalenga kutathmini matumizi ya kiteknolojia kupitia ufundishaji wa Kiswahili mkondoni katika chuo kikuu cha SEKU, kaunti ya Kitui.

Ingawa historia ya matumizi ya teknolojia kama vile tarakilishi katika ufundishaji wa lugha za Ulaya ni ya zamani, Auer na wenzake (2017) wanaeleza kwamba teknolojia haijatumiwa inavyostahili katika ufundishaji wa lugha. Kuhusu lugha ya Kiswahili, Michira (2017) na Mohochi (2016), wanaeleza kwamba ufundishaji wa Kiswahili kama LG kwa kutumia teknolojia umepewa nafasi ndogo.

Kwa kurejelea tafiti zilizotangulia, inabainika kwamba, ingawa watafiti wanakubaliana kwamba matumizi ya aina mbalimbali za kiteknolojia yana nafasi kubwa katika ufundishaji wa lugha ikiwemo lugha ya Kiswahili, tafiti hizo hazikujielekeza kuchunguza ufundishaji wa mkondoni kama nyenzo muhimu katika ufundishaji wa Kiswahili. Aidha, janga la UVIKO 19 lilichangia taswira mpya katika ufundishaji ambapo walimu walichangamkia ufundishaji wa mkondoni ili kukabiliana na changamoto ya kutoweza kutangamana na wanafunzi ana kwa ana. Ingawa nyenzo hii inaendelea kutumika, kuna tafiti chache hususan kuhusu ufundishaji wa Kiswahili mkondoni. Utafiti unaopendekezwa utaweza kuchangia maarifa mapya na kuziba pengo lililopo.

**Mafanikio ya elimu ya mkondoni katika kipindi cha UVIKO 19.**

Diocleciano (2022) ni mmoja wa wasomi waliojishughulisha na utafiti wa ufunzaji na ujifunzaji wa mkondoni. Yeye aliegemea mafanikio ya ufunzaji wa mkondoni katika kipindi cha janga la UVIKO 19 katika chuo kimoja nchini Zimbabwe.

Katika utafiti wake, Diocleciano alihusisha wanafunzi katika chuo lengwa. Yeye alilenga kueleza jinsi wanafunzi walivyochukulia suala la ujifunzaji na ufunzaji wa mkondoni. Kulingana na yeye (Diocleciano) wanafunzi hawakuridhishwa na ujifunzaji mkondoni hivyo mbinu hii haikufanikiwa kutokana na changamoto mbalimbali.

Diocleciano pia, katika utafiti wake, amezungumzia matatizo yaliyowakumba wanafunzi walipokuwa wakisoma kupitia mbinu ya mkondoni. Alieleza kuwa utafiti wake ulibaini kwamba ilikuwa vigumu kuwafanyia wanafunzi majaribio kujua ikiwa ufunzaji huu ulifanikiwa au la. Hivyo akapendekeza kwamba, ili kuondoa tatizo hili wahadhiri walihitaji kutumia video, jumbe, kutoa maelezo kwa njia ya mazungumzo, picha na kadhalika, kuhusu mada zilizofunzwa. Hili lingewasaidia wanafunzi kupanuka kimawazo na pia kuwa wabunifu.

Utafiti wa Diocleciano pia ulionyesha kwamba, mbinu hii ya mkondoni iliegemea upande mmoja ya ufunzaji. Yaani, walimu walituma makala tu kwa wanafunzi bila kuyatolea maelezo.

Hali hii iliwafanya wanafunzi kutokuwa makinifu katika utafiti na kuwa na fikira finyu.

Hata hivyo, utafiti wa sasa utakuwa tofauti sana na huu wa awali kwa sababu, yeye Diocleciano alijikita katika ufunzaji kwa jumla bila kuegemea somo maalumu. Utafiti wa sasa utaegemea ufunzaji mkondoni kwa kuzingatia lugha ya Kiswahili pekee yake. Pia, Diocleciano, alitafutia wakati maalum yaani kipindi cha uviko. Utafiti wa sasa, hutajikita katika wakati maalum bali ni kabla, wakati na hata baada ya UVIKO 19. Katika utafiti wa awali, watafitiwa ni wanafunzi peke yao; Utafiti wa sasa utalenga wanafunzi na hata walimu.

Utafiti huu pia ni tofauti na ule wa Diocleciano kwani, malengo yake pia ni tofauti. Yeye alilenga tu kutadhimini mafanikio na changamoto za ufunzaji wa mkondoni ila utafiti huu una malengo ya kutadhimini ufunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa undani.

Utafiti wa awali ulilenga wanafunzi wa kiwango cha vyuo nchini Zimbambwe, ila wa sasa unalenga Chuo Kikuu cha SEKU nchini Kenya.

**Usampulishaji**

Mtafiti alihusisha wanafunzi wanaosoma somo la Kiswahili na ambao wamesoma vipindi vya mkondoni pamoja na walimu wanaofundisha Kiswahili katika vyuo viwili (kikuu cha SEKU na kikuu cha Moi) nchini Kenya. Kutokana na uteuzi huu wa kinasibu, vyuo hivi vilihusishwa katika ukusanyaji wa data. Walimu wa Kiswahili waliohusishwa katika utafiti waliteuliwa kimakusudi. Walimu hawa waliteuliwa kimakusudi kwa kuwa wao wamehusika kwa ufundishaji mkondoni. Kwa hivyo, ilichukuliwa kwamba ni weledi wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa kutumia tarakilishi na vipakatalishi vikiunganishwa na vinuruweo. Walimu wote wanaofundisha Kiswahili kwa wanafunzi wa kila mwaka; mwaka wa kwanza, wa pili, watatu na wa nne,na hata uzamifu na uzamili,waliteuliwa kimakusundi kama kiwakilishi katika chuo kikuu cha SEKU kwa sababu walimu hao ni wachache. Wanafunzi waliolengwa katika utafiti huu walikuwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza, wa pili, wa tatu ,na wa nne. Pia wanafunzi wa uzamili na uzamifu walihusishwa. Hii ni kwa sababu utafiti ulilenga mada za sarufi,isimu na fasihi, zinazofundishwa katika viwango vyote

hivyo. Uteuzi wa sampuli kinasibu ulitumika kuwateua wanafunzi waliohusishwa katika ukusanyaji data. Wanafunzi waliteuliwa kinasibu ili kuwapa nafasi sawa ya kuhusishwa bila mapendeleo. Wanafunzi wa mwaka wa kwanza ni 174 kwa jumla. Hivyo, 20% yake ni wanafunzi 35, waliohusishwa. Mwaka wa pili kuna jumla ya wanfunzi 167. Hivyo, 20% itakuwa wanafunzi 33 walioshirikishwa. Mwaka wa tatu kuna jumla ya wanafunzi 122. Hivyo, 20% ya idadi hiyo ni wanafunzi 24 walioshirikishwa. Mwaka wa nne kuna jumla ya wanafunzi 78. Hivyo, 20% ya idadi hiyo ni wanafunzi 16 walioshirikishwa. Hii ina maana kuwa, wanafunzi 108 wa Kiswahili kati ya wanafunzi 541, kutoka mwaka wa kwanza hadi mwaka wa nne katika Chuo Kikuu cha SEKU walihusishwa katika utafiti huu. Pia, wanafunzi wote watano wa uzamili na saba wa uzamifu wanaosomea shahada ya uzamili na uzamifu mtawalia katika chuo kikuu cha SEKU walihusishwa.Hii ni kwa sababu,idadi yao ni ndogo.

**Kiwango cha Kutumia Masomo ya Mkondoni**

Wanafunzi waliulizwa kuonyesha kiwango cha matumizi ya masomo ya mkondoni katika chuo kikuu. Majibu yaliwasilishwa katika Jedwali 4.3.

**Jedwali 1 : Kiwango cha Utilizing cha Kutumia Masomo ya Mkondoni**

| Extent | Moi | | SEKU | |
|---|---|---|---|---|
| | **Mara** | **Asilimia** | **Mara** | **Asilimia** |
| Juu | 22 | 13.4 | 15 | 13.5 |
| Kawaida | 88 | 53.7 | 67 | 60.4 |
| Chini | 34 | 20.7 | 20 | 18.0 |
| Chini sana | 20 | 12.2 | 9 | 8.1 |
| **Jumla** | **164** | **100.0** | **111** | **100.0** |

.

Jedwali 1, linaonyesha kuwa wengi wa wanafunzi kutoka Moi (asilimia 53.7) na kutoka SEKU (asilimia 60.4) walionyesha kuwa walitumia masomo ya mkondoni kwa kiwango cha wastani. Hata hivyo, asilimia 20 ya wanafunzi kutoka Moi na asilimia 18.0 kutoka SEKU walionyesha kuwa walitumia masomo ya mkondoni kwa kiwango cha chini. Matokeo haya yanaonyesha kuwa wanafunzi walikuwa wakitumia mbinu ya masomo ya mkondoni.

Hii inakubaliana na utafiti wa Farrah na Al Bakry (2020) ambao walieleza kuwa wanafunzi walitambua faida nyingi za masomo mkondoni na walibaini changamoto zilizowakumba wakati wa mpito kutoka mbinu za jadi hadi mbinu za mkondoni. Pia walitoa mapendekezo ya kuboresha mbinu za ufundishaji mkondoni, kama vile kutoa vifaa vinavyohitajika na kuwapa Wahadhiri na wanafunzi mafunzo kwa ajili ya kujifunza na kufundisha kwa ufanisi mkondoni. Utafiti wao unahusiana na utafiti wetu kwa kuwa pia unalenga ufundishaji mkondoni, ingawa utafiti wao ulikuwa wa jumla bila kulenga somo maalum.

**Kiwango cha Kuridhika na Masomo ya Mkondoni**

Wanafunzi waliulizwa kuonyesha jinsi walivyoridhika na masomo ya mkondoni. Majibu yalionyeshwa katika Jedwali 2

**Jedwali 2: Kiwango cha Kuridhika na Masomo ya** Mkondoni

| Kiwango | Moi | | SEKU | |
|---|---|---|---|---|
| | **Mara** | **Asilimia** | **Mara** | **Asilimia** |
| Juu zaidi | 28 | 17.1 | 20 | 18.0 |
| juu | 84 | 51.2 | 64 | 57.7 |
| Wastani | 30 | 18.3 | 20 | 18.0 |
| Chini | 22 | 13.4 | 7 | 6.3 |
| **Jumla** | **164** | **100.0** | **111** | **100.0** |

Jedwali 2 linaonyesha kuwa wengi (asilimia 51.2) wa wanafunzi kutoka Moi na asilimia 57.7 kutoka SEKU walionyesha kuwa waliridhika na masomo ya mkondoni. Hata hivyo, asilimia 18.3 ya wanafunzi kutoka Moi na asilimia 18.0 kutoka SEKU walionyesha kuwa waliridhika kwa kiwango kidogo. Matokeo haya yanaonyesha kiwango cha juu cha kuridhika.

**Changamoto za kujifunza mkondoni kwa wanafunzi**

Wanafunzi walielezea changamoto kadhaa za masomo ya mkondoni kulingana na uzoefu wao. Wasiwasi mmoja wa kawaida ni kukosekana kwa mwingiliano wa ana kwa ana, ambao unaweza kusababisha hisia za upweke na kufanya iwe vigumu kujenga uhusiano na wenzake na Wahadhiri. Wanafunzi wengi wanakosa mambo ya kijamii ya masomo ya ana kwa ana, kama vile mazungumzo yasiyo rasmi na shughuli za kikundi zinazosaidia kujenga hisia ya jamii.

Tatizo lingine kubwa ni uwezekano wa kuingiliwa katika mazingira ya nyumbani. Wanafunzi wanaweza kupata ugumu wa kuzingatia masomo kutokana na usumbufu kutoka kwa jamaa na marafiki, wanyama wa nyumbani, au shughuli nyingine za nyumbani, ambazo zinaweza kuathiri uwezo wao wa kujihusisha kikamilifu na yanayofundishwa.

Changamoto za kiufundi pia zilitajwa mara kwa mara. Wanafunzi wanaweza kukumbana na matatizo ya kuunganishwa kwa

ISSN (Online): 2455-3662
EPRA International Journal of Multidisciplinary Research (IJMR) - Peer Reviewed Journal
Volume: 11| Issue: 8| August 2025|| Journal DOI: 10.36713/epra2013 || SJIF Impact Factor 2025: 8.691 || ISI Value: 1.188

mtandao, kasoro za programu, au kutokuwa na ujuzi na majukwaa ya mkondoni, ambayo yanaweza kuvuruga ujifunzaji wao na kuleta hasira. Zaidi ya hayo, si wanafunzi wote wana upatikanaji sawa wa teknolojia inayoaminika au nafasi tulivu ya kujifunzia, ambayo inasababisha tofauti katika uzoefu wa kujifunza.

Wanafunzi wengi waliripoti changamoto za kujituma na nidhamu. Urahisi wa masomo ya mkondoni unaweza wakati mwingine kusababisha ucheleweshaji, na kufanya iwe vigumu kubaki kwenye upeo na mipaka ya kiwakati. Kukosekana kwa muundo huu kunaweza kuleta msongo zaidi na wasiwasi, hasa kadri muda wa shughuli zima ya ujifunzaji unavyoyoma..

**Majibu ya Wahadhiri kuhusu matumizi ya mbinu za ufundishaji mkondoni**

Mtafiti aliwaomba Wahadhiri kuonyesha kiwango ambacho wametumia mbinu za ufundishaji mkondoni. Majibu yalitolewa katika Jedwali 3.

**Jedwali 3: Kiwango cha ufundishaji mkondoni**

| Kiwango | Mara | Asilimia |
|---|---|---|
| Juu | 2 | 22.2 |
| Kawaida | 6 | 66.7 |
| Chini | 1 | 11.1 |
| Chini sana | 0 | 0.0 |
| **Jumla** | **9** | **100.0** |

Jedwali 3 linaonyesha kuwa wengi (66.7%) wa Wahadhiri wa vyuo vikuu walionyesha kuwa kiwango ambacho walitumia ufundishaji mkondoni ni cha kawaida. Pia ilibainika kuwa 22.2% walikuwa wakitumia ufundishaji mkondoni kwa kiwango cha juu sana.

**Muhtasari wa Matokeo**

Matokeo yalionyesha kwamba, asilimia 90.2 ya wanafunzi walionesha kwamba waliohusika katika masomo ya mkondoni walikuwa na mtazamo chanya kuhusu masomo ya mkondoni, tofauti na asilimia 9.2 ambao walikuwa na mtazamo hasi. Kwa upande mwingine, asilimia 53.7 ya wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Moi na asilimia 60.4% kutoka SEKU walionyesha kwamba walitumia masomo ya mkondoni kwa wastani. Miongoni mwa wanafunzi, asilimia 51.2 ya wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Moi na asilimia 57.7% kutoka SEKU walionyesha kwamba waliridhika na masomo ya mkondoni. Wanafunzi waliripoti kwamba masomo ya mkondoni ni rahisi. Wanafunzi wanaweza kujifunza kwa kasi yao wenyewe na kwa ratiba zao wenyewe, na kuwapa nafasi ya kulinganisha masomo yao na kazi, wajibu wa kifamilia, au majukumu mengine. Uwezo huu unaweza kusababisha uzoefu wa kujifunza wa kibinafsi zaidi.

Wanafunzi walitaja changamoto kadhaa za masomo ya mkondoni kulingana na uzoefu wao. Wasiwasi mmoja wa kawaida ni ukosefu wa mawasiliano ya ana kwa ana, ambayo yanaweza kusababisha hisia za kutengwa na kufanya iwe vigumu kujenga uhusiano na wenzao na Wahadhiri.

Tatizo lingine kubwa ni uwezekano wa kuvurugika katika mazingira ya nyumbani. Wanafunzi wanaweza kukumbana na changamoto za kuzingatia kutokana na usumbufu kutoka kwa jamaa wa familia, wanyama wa nyumbani, au shughuli nyingine za nyumbani, ambazo zinaweza kuathiri uwezo wao wa kuhusika kikamilifu na vifaa vya kujifunza.

Tukio la kiufundi pia lilitajwa mara kwa mara. Wanafunzi wanaweza kukumbana na matatizo ya muunganisho wa mtandao, matatizo ya programu, au kutokuwa na ujuzi wa kutosha na majukwaa ya mkondoni, ambayo yanaweza kuharibu kujifunza kwao na kusababisha hasira. Zaidi ya hayo, si wanafunzi wote wana upatikanaji sawa wa teknolojia inayotegemewa au mahali pa kujifunzia tulivu, jambo linalopelekea tofauti katika uzoefu wa kujifunza.

Hata hivyo, wanafunzi walitaja faida zifuatazo za masomo ya mkondoni. Wanafunzi waliripoti kwamba masomo ya mkondoni ni rahisi. Wanafunzi wanaweza kujifunza kwa kasi yao wenyewe na kwa ratiba zao wenyewe, na kuwapa nafasi ya kulinganisha masomo yao na kazi, wajibu wa kifamilia, au majukumu mengine. Uwezo huu unaweza kusababisha uzoefu wa kujifunza wa kibinafsi zaidi.

Upatikanaji kwa urahisi, ni faida nyingine kubwa. Elimu ya mkondoni inaruhusu wanafunzi kupata masomo na rasilimali mbalimbali kutoka taasisi za ulimwengu mzima bila haja ya kuhama. Hii inafungua fursa kwa wale ambao huenda wakawa na tatitizo la kupata programu au masomo maalum katika eneo lao.

Zaidi ya hayo, masomo ya mkondoni mara nyingi yanatoa aina mbalimbali za vifaa vya kujifunza na rasilimali, kama vile video, maswali ya mwingiliano, na majukwa ya kujadili. Njia hii kuwa na nyenzo mbalimbali za mtandao,inasaidia kuwa na mitindo tofauti ya kujifunza, kusaidia wanafunzi kuhusika na maudhui kwa njia zinazowafaa zaidi.

Zaidi ya hayo, elimu ya mkondoni inaweza kusaidia kuboresha ujuzi wa teknolojia. Wakati wanafunzi wanaposhughulika na majukwaa na zana tofauti za kidijitali, wanakuwa na ujuzi zaidi na uwezo wa kubadilika katika kutumia teknolojia, ambayo ni faida muhimu katika soko la ajira la leo.

## MAREJELEO

1. *Davis, N. L., Gough, M., & Taylor, L. L. (2019). Online teaching: advantages, obstacles and tools for getting it right. Journal of Teaching in Travel & Tourism, 19(3), 256-263.*
2. *Kudzagi, Savious, Tarisayi na Everjoy, M. (2020), Matumizi ya WhatsApp kama suluhisho katika elimu wakati wa korona.*
3. *Msigwa, A. B. (2020). Mchango wa Media za Video katika Ufundishaji wa Kiswahili kwa Wageni. Mulika Journal, 38(1).*

4. *Ngesu, S. N. (2020). Nafasi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha va kigeni. Katika Kandagor M. (Mhr.) Kiswahili na Maendeleo ya Afrika. Taasisi za Taaluma za Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*
5. *Ngesu, S. N. (2021). Tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni nchini Uganda. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,*
6. *Vicent, S., & Msigwa, A. B. (2022). Umuhimu na Changamoto za TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili kwa Wageni. Mulika Journal, 40(2).*
7. *Zboun, J., & Farrah, M. (2021). Students' perspectives of online language learning during corona pandemic: Benefits and challenges.*